# The Best Insha
# KCPE 2008

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu juu ya kichwa kifuatacho:

MVUA YA GHARIKA KARIANI MWETU

Anza kwa: Wingu kubwa jeusi lilitokea upande wa mashariki. Baadaye matone mazito mazito ......

yalianza kunyesha. Ngurumo za radi zilihinikiza angani. Watoto walijawa na woga wa shumndwa. Fuadi wangu ulinidwikadwika mithili ya tokomire za wazaramo. Mvua yenyewe ilinyesha kwa fujo. Upepo mkali uliking'oa paa za nyumba. Tulikaa kimya na kutulia kama maji mtungini tusijue la kufanya. Chambilecho wamantiki na wananatiki wenye lisani za utaalamu na utalamidhi "Jambo usilolijua ni usiku wa giza.

Baada ya muwia wa kelbu kuukalia mkia, maji yalikuwa yamefurika furifuri na kuingia vyumbani vvyelu. Nilishikwa na huzuni kama mja aliyehukumiwa kunyonga, na sasa yuaongozwa katika kijia chenye giza, na hajui mambo yatakavyokuwa baada ya nukta chache.

Nilikuwa na wazazi wenye fulusi lukuki. Walinifunza na kunienzi kama mboni za maozi yao. Niliishi maisha ya raha mustarehe bimithili ya Sultan bin Jerehe. Sasa mali yetu yote yangesombwa na maji. Tulikimbia ili kuyaokoa maisha yetu. Mauti yalikuwa yakitukodolea mdozi. Wengine walibaki nyuma wakisema eti wao ni stadi wa kuogolea. Nasi tulikimbia kwani wahenga na wahenguzi wa jaai na jadudi hawakumlazimisha kiwete kuuparanga mti waliponadi "Kwa mwoga huenda kicheko na kwa shujaa huenda kilio.

Katika harakati zetu hizo, tulikutana na asadi wawili. Nilitetemeka bimithili ya kifaranga mwenye manyoya haba wakati wa kipupwe. Tulipambana

na hayawani hawa wawili na baadaye tukawashinda. kwani wahenga waligunga ndipo waliponadi" "Asiyeshindwa si mshindani."

Kwa bahati mbaya maji yaliongezeka na tukasombwa sisi sote. Hapa kila mtu alitumia ugwiji wake ili kuyanusuru maisha yake. Nilipiga bismillahi kwa Rabimsta ili anipe uwezo wa kuepukana na mauko haya. Baada ya muda wa tembe kumeza punje la mahindi, nilikuwa nchi kavu. Nilimshukuru Rabuka huku nikitumai ya kuwa Mungu si mfaki.

Kapu langu lilikuwa tupu na nilihitaji maankuli. Ghafla bin vuu nilisikia mgurumo wa magari. Loh! Niliona magari yaliyochorwa insalaba mwekundu. Nami nilikuwa nimejilaza ardhini kwani nilikuwa nimechoka hoi bin tiki tamthili ya punda wa dobi. Niliamka na kujikakamua hadi magari yalipotia habla. Walitoka kwenye gari huku wamevaa nguo za kupiga mbizi. Walinipea chakula nami nikala kwa ulafi kama majuniu wa majunju. Manusura waliokolewa na wengine wakapelekwa hospitalini. Tulipewa nguo, chakula na mablanketi. Tuliwasifu kwa wema wao kwani "chanda chema huvikwa pete

Baadaye, waliopatwa na mauko walipelekwa kwenye chumba cha kuhifadhia maiti. Mimi mwenyewe niligundua ya kuwa nilikuwa nimefiwa na wavyele wote wawili. Nililia kwikwikwi. Sikujua nianzie wapi na nimalizie wapi. Mawazo kochokocho yalinizunguka kichwani mwangu.

Wingu la jitimai lilitanda miongoni mwitu. Baadaye nilipelekwa kwa mbiomba wangu. Ndipo nilipoamini ya kuwa kifo hakina huruma hata chembe.

**(alama iliyotuzwa 38)**

Insha hii imeandikwa kwa ustadi mkubwa. Kazi imepangwa vizuri kwa sentensi na aya pamoja na hati inayovutia. Makosa ya aina yoyote ni machache sana. Mtahiniwa amejaribu kueleza yaliyotokea akizingatia mada aliyopewa. Hoja zake zimekamilika, na insha yake ameikoleza utamu kwa matumizi ya semi na tamathali. Kosa la tahajia limeonakana:
Mwitu – mwetu

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

- Ni vizuri mfundishe Kiswahili kwa ujumla wake. Tumieni vitabu ambavyo vimependekezwa na Wizara ya elimu katika kufundisha.
- Sisitizieni wanafunzi kuwa wakijibu maswali ya kifungu ni lazima wasome kifungu chote ili waweze kujibu maswali, wala wasijikite pale wanapofikiria kuwa swali limetoka.
- Wanafunzi wenu ni lazima wasome kichwa cha insha na kuelewa mada ili waweze kutoa hoja nyingi. Wafundisheni mbinu ya kuzindondoa hoja zao kwanza na kuzikuza katika aya.

Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel: +254734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com |

ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com